# Dr Mbennah: Leadership
# AIC(T) Dayosisi ya Pwani

WARSHA YA WAINJILISTI NA WAKE/WAUME ZAO

Chuo cha Ujenzi Morogoro
9-13 Novemba 2009

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 Asanteni sana kunikaribisha kushirikiana nanyi

1.2 Tutaangalia mambo mbalimblai muhimu yanayohusiana na uongozi katika huduma za Kikristo

1.3 Kwa nini kujifunza uongozi? Uongozi ni muhimu. Jeshi la simba linaloongozwa na kondoo ni jeshi lililoshindwa katika vita; jeshi la kondoo linaloongozwa na simba ni jeshi lililokwishashinda vita. Hapa ni suala la uongozi!

## 2.0 KIINI CHA UONGOZI

2.1 Uongozi ni nini?

2.2 Kiongozi ni nani?

2.3 Kwa nini kuna uongozi? Au kwa nini uongozi unahitajika?

## 3.0 MISINGI YA UONGOZI

3.1 Uongozi hasa ni uongozi wa kiutumishi

3.1.1 Kuna aina mbalimbali za uongozi

3.1.2 Uongozi wa kidunia unajihusisha sana na cheo na ukubwa wa kiongozi binafsi (Linganisha na Yohana 13:1ff)

3.1.3 Uongozi wa kidunia unaendeshwa kwa mamlaka na nguvu (Linganisha Luka 22:25) – *power of position*!

3.1.4 Uongozi wa kidunia umejawa na tama ya fahari – watu wanapenda kuitwa wakuu au mabwana na kuitwa kwa vyeo vyao (Luka 22:25)

3.1.5 Uongozi wa kiroho hauhusudu *seniority*

3.1.6 Uongozi wa kiroho unatekelezwa kwa utumishi (Linganisha Luka 22:26). Kiongozi awe mtumishi wa wote. Kutumika ni kutoa, siyo kupokea. Baadhi ya mambo yanazuia uongozi wa kitumishi ni kiburi, kujihisi kuwa siyo salama (*insecurity*). Yesu: Kilele cha uongozi wa kiutumishi (Linganisha Yohana 13, Marko 10:45, Luka 22). Watu wengi wanataka kumtumikia Bwana Yesu lakini hawako tayari kuwatumikia watu wengine.

3.2 Uongozi ni tofauti na utawala

3.3 Uongozi ni suala na tabia ya mtu – *character*, siyo matendo tu

3.3.1 Mungu anaangalia moyo – tabia

3.3.2 Watu wanaoongozwa wanaangalia tabi

3.3.3 Tabia ndio msingi wa kufanikiwa au kutokufanikiwa katika uongozi

3.3.4 Yapasa kujenga tabia ipasayo, ili kuwa kiongozi hasa

**4.0 MAJUKUMU YA KIONGOZI**

4.1 Kuongoza! Kufanya maamuzi (kufanya, kwa haki, kwa wakati, kwa hekima, kwa sifa na utukufu wa Mungu)

4.2 Kulea na kukua viongozi wengine (*mentoring*)

4.3 Kuwezesha wenginge kutekeleza majukumu yao (*supporting/enabling*)

4.4 Kuandaa watu wa kuchukua nafasi yake (*succession planning*)

4.5 Kuwajenga wengine hata wapate kujua na kulitumikia kusudi la Mungu kwa maisha yao (kama Mordekai)

**5.0 SIFA MUHIMU ZA KIONGOZI**

5.1 Moyo wa kiongozi

5.2 Kuwa na maono ya kiMungu na kuyatumikia

5.3 Ujasiri

5.4 Kuwa na kina kinachoongezeka cha uhusiano sahihi na Mungu

5.5 Kudumisha tabia za kiroho (maombi, kukua katika Neno la Mungu, kupenda haki na kweli, kushuhudia Yesu na upendo wake kwa wote)

5.6 Unyenyekevu na kuvunjika

- 5.1 Thamani yetu huongezeka kadiri tunavyovunjika
- 5.2 Maana yake ni kujiachia kabisa na kujikabidhi kwake Kristo (atakaye kunifuata, ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku anifuate)
- 5.3 Kuvunjika kunadai “kufa” – msalaba ni alama ya kufa, kufa nafsini, kila siku.

5.7 Uwezo wa kuwasiliana kikamilifu

5.8 Kudhihirisha hali tabia ya Bwana Yesu (kwa maadui, kwa wanawake, kwa watoto, na kwa makundi ya watu yasiyokubalika katika jamii)

5.9 Identity katika Kristo

**6.0 KANUNI ZA UONGOZI WENYE UFANISI**

6.1 Matumizi sahihi ya ulimi. Katika kuongoza tunalazimika kusema mengi katika mazingira mbalimbali. Haya ni matumizi ya ulimi. (Kama ungerekodi kila neno ulilosema juma zima kisha siku ya Jumapili uwape fursa watu kanisani kusikiliza, ungelijisikiaje?)

6.2 Maneno yako yana nguvu na uwezo wa kuhuisha au kuangamiza (tazama Mithali 18:21. Kitabu cha Mithali kina mistari ipatayo 900. Kati ya hiyo, zaidi ya mistari 100 inazungumzia kusema. Angalia mistari mingine: Mathayo 12:36; Waefeso 4:29.

- 6.2.1 Mambo yasiyopaswa kutoka kwenye vinywa vyetu: neno lililo ovu: uwongo (directly, or creating false impression, or exaggeration), maneno yaliyosemwa katika hasira na uchungu, maneno machafu au maneno ya mzaha hasa yanayohusiana na viungo vya mwili wa mwanadamu (Waefeso 5:4), mazungumzo ya kipuuzi (linganisha 2 Timotheo 2:23), aina fulani za utani, kuwa na maneno mengi (Mithali 10:19, penye maneno mengi, dhambi haikosekani); tazama pia 2 Timotheo 2:16; Yakobo 1;19; Mhubiri 5:13 (usiseme maneno mengi mno mbele za Mungu), maneno ya kujipendekeza (flattery) (tazama Mithali 26:28), kuapa, kusengenya (1 Timotheo 5:13; Mithali 16:28, 18:8), kusingizia.

6.2.2 Mambo yanayokubalika kutoka katika vinywa vyetu: Maneno ya kuwabariki na kuwajenga wengine – wajione wanapendwa au wanakubalika au wanathaminiwa au wanatambuliwa tu. Yapasa yawe maneno ya kuwanufaisha wanaokusikiliza.

6.2.3 Ili ulimi ubadilike: Yapasa kutubu dhambi ya ulimi, kumwomba Mungu abadili moyo (linganisha Luka 6:45), kushika mistari ya Biblia moyoni au kujaza moyo na neno la Mungu (linganisha Zaburi 119:9, 11; Waefeso 4:29), hasa shika mistari inayohusu tatizo ulilo nalo; na kumpa Mungu nafasi ya kufanya mabadiliko ya tabia ya usemi.

6.3 Matumizi sahihi ya mamlaka

6.4 Kuwa na kawaida na mikakati stahiki ya kuendelea kukua kiroho na kihuduma, na kujiendeleza kkielimu, kiuongozi, na kiuchumi.

6.5 Kuwa na tabia na moyo wa kusamehe

6.6 Kumaliza safari ya uongozi vema

6.6.1 Mfalme Sulemani alianza vizuri sana, lakini hakumaliza vizuri (tazama1 Wafalme 3:1 – 11:14). Sulemani alimpenda Mungu (3:3), kwa sababu hiyo akaipewa nafasi ya kuomba chochote (3:5), aliomba hekima ili awaongoze vema watu wa Mungu (3:9), kwa sababu alikiri kwamba yeye mwenyewe asingeweza (3:7, 8). Mungu alimpa hekima (3:12) na zaidi (3:13, 14) lakini kwa masharti kwamba Sulemani angezifuata Njia za Mungu na maagizo ya Mungu.

6.6.2 Mfalme Uzia alianza vizuri sana, lakini hakumaliza vizuri (2 Mambo ya Nyakati 22). Tazama mst 3-5; 6-15; 16-19.

6.6.3 Mungu aliendelea kuwafanikisha hawa wawili hadi hapo walipoacha kushika Njia zake na kufuata maagizo yake. Mungu alimfanikisha sana Sulemani (tazama 1 Wafalme 3:28-10:25; na pia Mhubiri 2:4-10). Lakini unafika wakati hali ya Sulemani inaonekana kubadilika na kuwa mbaya kwa haraka sana. Wote Sulemani na Uzia walisahau agizo la Mungu kwa wafalme wa Israeli katika Kumbukumbu la Torati 17:14-20. Lakini Sulemani alikiuka agizo hili: Tazama 1 Wafalme 10:23-11:14. Katika 10:23 tunasoma kwamna Sulemani alitajirika sana kupita wote; 10:28 tunasoma kwamba Sulemani aliagiza farasi kutoka Misri, na 11:1-8 tunasoma kwamba Sulemani aliwapenda wanawake wengi wa mataifa.

Kwa upande wake, Uzia aliendelea vema mpaka alipoanza kujiona kuwa ni mwenye nguvu, baada ya kuwashinda mataifa mengine katika vita, na kufanikiwa kujenga ngome na minara, na kufanikiwa katika kilimo na kuwa na jeshi kubwa. Mst 16: Uzia akawa mwenye nguvu na kiburi kinamletea maanguko, na akaacha kufuata maagizo ya Mungu (tazama mst 17-19).

6.6.4 Mambo yatakayoleta maanguko ya kiongozi

Mungu ametupa vipawa na karama na uwezo na ujuzi mbalimbali, Shetani hupenyeza kutuangusha kupitia vitu hivyo vyema ambavyo Mungu ametupatia.

Kujiona na kuwa kiburi kinachotokana na kujiona au kutambua uwezo tulio nao: Watu wanapoguswa na maisha yao kubadilika kutokana na huduma yetu na hudma inapozid kupanuka ni mazingira yanayoweza kuvutia kuchipuka kwa kiburi.

Utelezi wa mafanikio, hasa mafanikio ya kihuduma

Kumsahau Mungu, na huko alikotutoa (linganisha Kumbukumbu la Torati 8:10-18). Mungu anatambua hatari ya mafanikio ndio maana anatuonya hapa.Kila mtumishi na kiongozi atajaribiwa kumsahau Mungu baada ya kupata mafanikio makubwa.

Kujitengenezea kanuni ya maisha na uongozi au utumishi, kama Mfalme Uzia alivyofanya. Viongozi wengi baada ya mafanikio wanajiandikia kanuni zao wenyewe

mpya za maadili, za tabia ya kazi, za mtazamo wa watu, za kufunga na kuomba, kanuni za utajiri na mali, na wanafafanua viwango tofauti na mafundisho ya Biblia

Kutafuta maana ya maisha na utambulisho wako katika huduma, na kuacha kujitambua kama mtoto wa Mungu. Kufafanua utu kwa kigezo cha ukubwa, upana, na ubora wa huduma. Kuwa mkubwa katika huduma.

Dhambi inayofuata (tazama 1 Timotheo 5:24, 25)

## 7.0 CHANGAMOTO KATIKA UONGOZI

7.1 Kiongozi na familia (kudumisha uwiano sawia) – upana wa huduma na moto wa huduma kunyang'anyana muda na familia (mke/mume na watoto). Matumizi yasiyo sahihi ya Mathayo 6:33 na Mathayo 10:37. YAPASA kukumbuka 1 Timotheo 3:4, 5)

7.1.1 Kanuni ya 1: Uongozi wa familia ni sharti la kuwa kiongozi katika kanisa au huduma yoyote ya kiroho.

7.1.2 Kanuni ya 2: Uongozi wa familia ni maandalizi ya uongozi katika kanisa au huduma yoyote ya kiroho

7.1.3 Kanuni ya 3: Uongozi wa familia unatangulia uongozi katika kanisa au katika huduma yoyote ya kiroho. Mathayo 10:37 haihusu uhusiano kati ya huduma na familia, bali kati ya familia na uhusiano wa mtu na Yesu Kristo.

7.2 Yapasa kuweka kipaumbele katika uongozi wa familia: muda na mume au mke (vinginevyo na kuwa na uhusiano wa kindoa na huduma), muda na watoto, na muda na familia nzima. Yapasa kukumbuka ya kwamba kazi ya Mungu itaendelea hata bila sisi, lakini familia zetu hazitaendelea bila sisi.

7.3 Majaribu (mamlaka, fedha, mapenzi)

7.4 Ugumu na upana wa kazi na kwa hiyo uchovu na matatizo ya kiafya

7.5 Kushughulika kikamilifu na pande mbalimbali zisizofanana

7.6 Udikteta wa kidemokrasia

7.7 Hali ngumu ya kiuchumi

7.8 Kuongoza watu wanaokuzidi kiupeo, kielimu, kiroho au kiuzoefu

## 8.0 HITIMISHO

Mwombe Mungu akudumishe katika kuendelea vema, hadi umalize vizuri

Mwombe Mungu akurejeshe katika nafasi uliyoanza nayo

UONGOZI KATIKA HUDUMA ZA KIKRISTO
Rev Dr E D Mbennah
TWR International
Africa Region
PO Box 4232 Kempton Park 1620
SOUTH AFRICA
E-mail: mbennah@yahoo.com OR embennah@twraro.org.za